# Maisha Ya Mkristo Ni Nini?

**na**

**Ellis P. Forsman**

# Maisha Ya Mkristo Ni Nini?

**na**

**Ellis P. Forsman**

**Oktoba 17, 2011**

# Maisha Ya Mkristo Ni Nini?

## Math. 16:24-28

Wengi wanakubali wazo la Ukristo bila kujua maana yake ya kweli. Kwa baadhi, wazo la Ukristo ni kubatizwa pekee.

Na kwa wengine, wazo la Ukristo ni kwenda tu kanisani. Bali kwa wengine, wazo la Ukristo ni kuwapendeza familia zao au majirani zao tu.

Ukristo wa kweli ni zaidi ya hayo – ni kuishi maisha ya kipekee.

Mkristo wa kweli anajitoa mwenyewe kwa Bwana.

Math. 16:24, "*Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe ajitwike msalaba wake anifuate.*"

Mkristo wa kweli hafanyi kile kinacho mpendeza kufanya, lakini badala yake anafanya kile kinacho mpendeza Mungu.

- Waru. 6:17-18, "*Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki.*"

- Waru. 10:1-3, "*Ndugu zangu nitakayo sana moyoni mwangu, na dua yangu nimwombayo Mungu ni kwa ajili yao ili waokolewe. Kwa maana nawashuhudia kwamba wana juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si katika maarifa. Kwa maana ikiwa hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu.*"

- Waru. 15:3, "*Kwa maana Kristo naye hakujipendeza mwenyewe…*"

Hata hivyo Petro alikuwa na wazo zuri la kujenga vibanda vitatu, moja kwa ajili ya Musa, moja kwa ajili ya Eliya, na nyingine kwa ajili ya Yesu. Mungu hakupendezwa na hili kwa sababu Petro hakujitoa mwenyewe kwa maneno ya Yesu, lakini badala yake akaja na mawazo yake mwenyewe.

Lakini Mungu alipendezwa na Kristo. Math. 17:5, "*Alipokuwa katika kusema tazama wingu jeupe likawati uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye.*"

Katika somo hili tunakwenda kuangalia aina ya maisha maalum inayompendeza Mungu.

# Ukristo ni maisha iliyozungukwa

## Ayubu alifurahia ukigo la Mungu kuhusu yeye.

Ayu. 1:10, "*Wewe hukumzingira kwa ukigo pande zote, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Kazi za mikono yake umezibarikia, nayo mali yake imeongezeka katika nchi.*"

Mungu hakukataa ukigo huu kwa sababu kwanza Ayubu aliishi maisha ambayo yalimpendeza Mungu badala ya kuishi maisha ya kumpendeza mwenyewe.

Mungu alafu akamruhusu shetani kumjaribu Ayubu, lakini bado alitunza ukigo kwa ajili yake ili kulinda maisha yake.

Ukigo huu haukuwa wa kimapambo, bali ulimzunguka Ayubu ili kumlinda.

## Maisha ya Ukristo leo ni maisha yaliyozungukwa.

Waef. 2:8, "*Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu.*"

Neema ya Mungu inatufunika tunapoishi maisha yanayompendeza. Neema ni zaidi ya Kristo kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu; ina jumuisha mpango wote wa Mungu wa wokovu.

- Tito 2:11-12, "*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tama za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa.*"

- Waru. 1:16-17, "*Kwa maana siionei haya injili kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.*"

## Yesu Kristo na Neema yake ni kuu kuliko ulimwengu.

- 1 Yohana 4:4, "*Ninyi watoto wadogo mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia.*"

- 1 Yohana 2:1, "*Watoto wangu wadogo nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki.*"

**Lakini haimaanishi kwamba tuendelee kutenda dhambi makusudi.**

Waru. 6:1-4, "*Tuseme nini basi tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"

**Neema ya Mungu inatuzunguka na kutulinda pale ambapo kweli tunalipenda neno la Mungu, na kuliweka salama mioyoni mwetu, na kujaribu kuishi kwalo.**

Zaburi 119:11, "*Neno lako nimeliweka moyoni mwangu, ili kwamba nisikutende dhambi.*"

# Ukristo ni maisha ya utumishi

## Watu wengi wanapenda kutumikiwa badala ya kuhitaji kutumika.

**Mfano mkuu wa utumishi ni Mkuu wetu, Yesu.**

Marko 10:45, "*Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.*"

**Paulo alimtumikia Mungu.**

Matendo 27:23, "*Kwa maana usiku huu wa leo malaika wa Mungu yule ambaye mimi ni wake, naye ndiye nimwabuduye, alisimama karibu name.*"

**Wakristo wanatakiwa kuwa watumishi, pia.**

- Wagal. 6:10, "*Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio.*"
- Math. 10:42, "*Na mtu awaye yote atakayemywesha mmoja wapo wa wadogo hawa ngaa kikombe cha maji ya baridi, kwa kuwa ni mwanafunzi, amin, nawaambia, haitampotea kamwe thawabu yake.*"

## Baadhi ya watu wasio na furaha wanasema, “Niko hapa, nitumikie!”

**Tunatakiwa tuwe na tabia ambayo Paulo alikuwa nayo kabla ya kuongoka kwake.**

Matendo 9:6, “*Lakini simama uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda.*”

**Yesu alimaliza kazi Yake kama mtumishi wa Mungu.**

Yohana 17:4, “*Mimi nimekutukuza duniani hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye.*”

**Tunapotimiza wajibu wetu kama watumishi, matendo yetu yatatufuata.**

- Ufu. 14:13, “*Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya tabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao.*”
- Ufu. 20:12, “*Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo wamesisimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.*”

# Ukristo ni maisha ya kiroho

## Tunapaswa kutembea kiroho.

- Yohana 4:23-24, “*Lakini saa inakuja nayo sasa ipo ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafu watu kama hao wamwabudu. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*”
- Waru. 8:1-5, “*Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho. Kwa maana wale*

*waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho.*"

Tunapaswa kuishi maisha katika mwili, lakini si kwa kuutegemea.

## Inamaanisha nini kuishi maisha kwa kuufuata Roho?

**Kusulubisha (kuua) katika maisha yetu tama za mwili.**

- Wagal. 2:20, "*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai niliyo nao sasa katika mwili ninao katika imani ya Mwana wa Mungu ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*"
- Waru. 8:13, "*Kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa, bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho mtaishi.*"
- 1 Petr. 2:11, "*Wapenzi nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tama za mwili zipinganazo na roho.*"

**Kuweka ufalme wa Mungu kwanza katika maisha yetu.**

Math. 6:33, "*Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake, na haya yote mtazidishiwa.*"

Hiyo ni, vitu ambavyo vinahitajika, siyo kimsingi vitu tunavyotaka.

# Ukristo ni maisha yanayong'aa

## Wakristo lazima wawe mwanga wa Mungu.

- Yohana 8:12, "*Basi Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.*"
- Math. 5:14, "*Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu yam lima.*"

## Wakristo lazima wang'ae kama nuru ya ulimwengu.

Wafil. 2:15, "*Mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka; ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu.*"

Ishi kama mfano wa jinsi ambavyo Mkrisro mwema anavyopaswa kuishi.

# Ukristo ni maisha ya furaha

## Lazima tupende kuishi maisha ya kiroho.

1 Petr. 3:10, "*Kwa maana atakaye kupenda maisha, na kuona siku njema, auzuie ulimi wake usinene mabaya, na midomo yake isinene hila.*"

Mungu anataka watoto wake wawe na furaha, hata katika mazingira magumu.

**Paulo na Sila walikuwa mfano wa kuwa na furaha wakati wa majaribu.**

Matendo 16:19-25, "*Basi bwana zake walipoona ya kuwa tumaini la faida yao limewapotea, wakawakamata Paulo na Sila, wakawakokota mpaka sokoni mbele ya wakuu wa mji; wakawachukuwa kwa makadhi, wakasema watu hawa wanachafua sana mji wetu, nao ni Wayahudi; tena wanatangaza habari ya desturi zilizokuwa halali kwetu kuzipokea wala kuzifuata, kwa kuwa sisi tu Warumi. Makutano wote wakaondoka wakawaendea, makadhi wakawavua nguo zao kwa nguvu, wakatoa amri wapigwe kwa bakora. Na walipokwisha kuwapiga mapigo mengi, wakawatupa gerezani, wakamwamuru mlinzi wa gereza awalinde sana. Naye akiisha kupata amri hii akawatupa katika chumba cha ndani, akawafunga miguu kwa mkatale. Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza.*"

**Petro na mitume wengine walikuwa mifano ya kuwa na furaha wakati wa majaribu.**

Matendo 5:26-42, "*Ndipo yule jemadari akaenda pamoja na watumishi wakawaleta, lakini si kwa nguvu kwa maana waliogopa watu wasije wakawapiga kwa mawe. Walipowaleta wakawaweka katika baraza. Kuhani Mkuu akawauliza, akisema, Je! Hamkuwaamuru ninyi kwa nguvu, msifundishe kwa jina hili? Nanyi, tazameni, mmeijaza Yerusalemu kwa mafundisho yenu, na mnataka kuileta damu ya mtu yule juu yetu. Petro na mitume wakajibu, wakisema, Imetupasa kumtii Mungu kuliko mwanadamu. Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu, ambaye ninyi mlimwua mkimtundika katika mti. Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi. Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio. Wao waliposikia wakachomwa mioyo yao; wakafanya shauri kuwaua. Lakini mtu mmoja Farisayo, jina lake Gamalieli, mwalimu wa torati mwenye kuheshimiwa na watu wote, akasiamama katika baraza, akaamuru mitume wawekwe nje kitambo kidogo, akawaambia, Enyi waume wa Israeli, jihadharini jinsi mtakavyowatenda watu hawa. Kwa sababu kabla ya siku hizi aliondoka*

*Theudi, akijidai ya kuwa yeye ni mtu mkuu, watu wapata mia nne wakashikamana naye; naye aliuawa na wote waliomsadiki wakatawanyika wakawa si kitu. Baada ya mtu huyo aliondoka Yuda Mgalilaya, siku zile za kuandikwa orodha, akawavuta watu kadha wakadha nyuma yake, naye pia akapotea na wote waliomsadiki wakatawanyika. Basi sasa nawaambia, jiepusheni na watu hawa, waacheni kwa kuwa shauri hili au kazi hii ikiwa imetoka kwa binadamu, itavunjwa, lakini ikiwa imetoka kwa Mungu hamwezi kuivunja; msije mkaonekana kuwa mnapigana na Mungu. Wakakubali maneno yake; nao walipowaita mitume, wakawapiga, wakawaamuru wasinene kwa jina lake Yesu; kisha wakawaacha waende zao. Nao wakatoka katika lile baraza, wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo. Na kila siku ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo.*"

Manabii wa zamani waliteseka, lakini bado walichukuliwa kuwa na furaha.

Yakobo 5:10-11, "*Ndugu, watwaeni manabii walionena kwa jina la Bwana, wawe mfano wa kustahimili mabaya, na wa uvumilivu. Angalieni twawaita heri wao waliosubiri. Mmesikia habari ya subira yake Ayubu, mmeuona mwisho wa Bwana ya kwamba Bwana ni mwingi wa rehema, mwenye huruma.*"

**Sisi pia tunapaswa kuwa na furaha tunapoteseka kwa kufanya kazi ya Bwana.**

- 1 Petr. 3:12-14, "*Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yake huyasikiliza maombi yao; bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya. Naye ni nani atakayewadhuru, mkiwa wenye juhudi katika mema? Lakini mjapoteswa kwa sababu ya haki mna heri. Msiogope kutisha kwao, wala msifadhaike; bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu.*"

- 1 Petr. 4:12-16, "*Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. Lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe. Mkilaumiwa kwa ajili ya jina la Kristo ni hari yenu; kwa kuwa Roho wa utukufu na wa Mungu anawakalia. Maana mtu wa kwenu asiteswe kama mwuaji, au mwivi, au mtenda mabaya, au kama mtu ajishughulishaye na mambo ya watu wengine. Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu kwa jina hilo.*"

Jishughulishe kama Mkristo na furaha itakufuata.